

HALMASHAURI YA MANISPAA SONGEA

MKOA WA RUVUMA

PHONE NUMBER-2602970



UKUMBI WA MANISPAA
P.O. BOX 14,
SONGEA.

TANGAZO LA UUZAJI WA VIWANJA KWA BEI YA SERIKALI ENEO LA LILAMBO NDANI YA MANISPAA YA SONGEA

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Songea anawatangazia wananchi wote kuwa anauza viwanja vilivyopimwa katika eneo la Lilambo kwa ajili ya viwanda vidogo, viwanja hivyo vipo mkabala na barabara ya Songea – Mbinga, umbali wa kilomita 12 kutoka katikati ya Mji wa Manispaa ya Songea. Miundombinu wezeshi (maji, Barabara ya Lami na umeme) ipo kwenye eneo la mradi. Aidha barabara zote za ndani ya mradi zitachongwa na zitapitika wakati wote. *(viwanja hivi vipo karibu na eneo la kiwanda cha ndugu. Savio)*

Fomu za maombi zinapatikana katika Ofisi ya Idara ya Ardhi na Mipango Miji ya Halmashauri ya Manispaa ya Songea kuanzia saa 3:00 asubuhi hadi saa 9:00 alasiri siku za kazi kuanzia Jumatatu hadi Ijumaa. Bei ya fomu inapatika kwa shilingi 20,000/= kwa kila fomu moja ambayo hazitarudishwa.

Bei ya viwanja kwa kila mita ya mraba ni kama ifuatavyo:-

Na	Matumizi	Bei elekezi kwa mita moja ya mraba
1.	Viwanda vidogovidogo	2,000/=
2.	Viwanda Vya Kati	2,000/=
3.	Makazi	2,000/=
4.	Biashara	2,000/=

Ukichagua kiwanja chenye mita mraba 1300 x 2,000/= utalipa Tshs. 2,600,000/=

Ukichagua kiwanja chenye mita mraba 3000 x 2,000/= utalipa Tshs. 6,000,000/=

Bei hizi ni ghaarama za manunuzi hivyo utagharamia gharama za umilikishaji na kodi ya ardhi ya kila mwaka.

WANANCHI WOTE MNAKARIBISHWA KUNUNUA VIWANJA VILIVYOPIMWA NA VYENYE HATI

Tangazo hili limetolewa leo tarehe 15/10/2018 na:

MKURUGENZI WA MANISPAA
SONGEA